


VITA VYA VIJUJI



HATA VITA VINA MIPAKA

KAMATI YA KIMATAIFA YA MSALABA MWEKUNDU



ICRC

UTANGULIZI

"Upepo wenye kasi
hauondelei mbali kila kitu"
(Methali ya Kipokot, Kenya)

Wasomaji Wapendwa,

Vita hutokea kote duniani na wakati mwingine huonekana kama hakuna jambo lolote linaloweza kuzuia utumiaji nguvu. Hata hivyo, lazima tukumbuke kwamba hata vita vina mipaka! Katika kila nchi, dini na utamaduni, tunapata sheria na mila zenye lengo la kupunguza madhila yanayosababishwa na vita. Kanuni hizi ndizo kiini cha Sheria ya kibinadamu ya Kimataifa, kundi la kanuni za ulimwengu zinalolinda wanaokumbwa na vita, hasa watoto na wanawake, na kuwazuia wapiganaji wasitumie silaha fulani.

Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (ICRC) inawasaidia wanaokumbwa na vita kote duniani na inashughulika na kulinda haki zao na heshima yao. Mateso ya binadamu yanayosababishwa na vita ndiyo mada ya kitabu hiki cha hadithi kwa picha. Hadithi inahusu jumuiya mbili, Wazuta na Waama ambao wanaishi katika vijiji tofauti. Kwa kuwa Wazuta na Waama wanashindwa kuishi pamoja kwa amani, wanatumia nguvu na kusababisha mateso mengi katika vijiji vyao viwili. Je, wataendelea hivyo mpaka lini? Je, wataweza kupata njia za kupunguza athari za vita vyao?

Kwa kweli Waama na Wazuta si jamii halisi, lakini matukio kama hayo yanapatikana katika maeneo ya kivita kote duniani. Je, tutafanya nini kuhusu hali hiyo? Soma hadithi hii halafu ujadiliane na marafiki zako kuhusu hatua unazoweza kuchukua katika hali ya namna hiyo. Kwa maoni yako, ni jambo gani linaloweza kufanywa ili kupunguza mateso kwa wanaokumbwa na vita? Sisi katika ICRC tunaamini kwamba, kila mmoja wetu ana chaguo, lile la maisha na heshima ya binadamu. Tunatumai kuwa utakubaliana na kuungana nasi katika kueneza mawazo haya muhimu sana.

Mwishoni mwa kitabu hiki, utapata michezo na taarifa zaidi kuhusu Msalaba Mwekundu na shughuli zake.

Furahia hadithi!

Vincent Nicod
Mkuu wa Ofisi ya Nairobi ya ICRC

MICHANGO

Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu ingependa kuwashukuru wafuatao kwa msaada na mchango wao katika kutayarisha kitabu hiki cha hadithi kwa picha:

Wizara ya Elimu (Kenya) na Walimu na Wanafunzi wa:

Shule ya Msingi Pitpagh (Pokot Magharibi), Shule ya Msingi Sangach (Marakwet), Shule ya Msingi Kolloa (Baringo Mashariki) Shule ya Msingi Imonpoquet (Pokot Magharibi), Shule ya Msingi Kapsangar (Pokot Magharibi) Shule ya Msingi Kipteber (Marakwet) Shule ya Msingi Gatanyaga (Thika) Shule ya Msingi Ngoriba (Thika) na Shule ya Msingi ya Limuru (Limuru Model Primary School).

UTOAJI:

Kitabu cha "Vita vya Vijiji" kimetolewa na Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu, Ofisi ya Nairobi, 2002.

Mratibu wa Mradi: Vincent Bernard, Ofisa Mawasiliano, Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (ICRC).

Kazi ya Utafiti na Uhariri: Emmanuel Nyabera, Ofisa Usambazaji na, Florian Westphal, Ofisa Habari wa Kanda, ICRC.

Uandishi wa Makala & Uelekezi wa Sanaa: Nduhiu Change, Artage Communications.

Michoro: Henry Koske, Artage Communications.

Michoro ya Kompjuta: Davidson Njoroge, Artage Communication.

Majaribio na Utafiti: Eva Slater, Artage Communications, Anne Kilimo na Robin Waudo, Maafisa Mawasiliano, ICRC, na Lucy Chai, Msaidizi wa Mawasiliano, ICRC.

Mtafsiri kwa lugha ya Kiswahili: The National Kiswahili Council, United Republic of Tanzania.

Mhariri wa tafsiri ya Kiswahili: Dkt. Kithaka wa Mberia.

VITA VYA VUWI

Habari kuhusu Sheria ya Binadamu ya Kimataifa iliyochapishwa na
Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu



Uandishi wa Makala & Uelekezi wa Sanaa: *nduhui Change*
Michoro: *henry Koske*
Michoro ya Kompyuta: *davidson Njoroge*



ICRC

T2002.080/400

BAADHI YA WAHUSIKA WALIOMO KATIKA HADITHI



HANNA



YOHANA



JUMA



MARIA



BI. MUSA



BW. MUSA



MAMA KUTOKA
AMA



MFANYIKAZI WA
MSALABA MWEKUNDU.



MTEMI WA
KIJIJI CHA ZUTA



MTEMI WA
KIJIJI CHA AMA



MWANAUME
MWENYE HASIRA
KUTOKA AMA



MPIGANAJI
KUTOKA ZUTA



MPIGANAJI
KUTOKA ZUTA



MPIGANAJI
KUTOKA ZUTA




MPIGANAJI
KUTOKA ZUTA


KIJIJI KIDOGO CHA AMA KINAKUWA KIMYA KADRI USIKU UNAVYOINGIA. WANAKIJIJI WANAKIMBILIA NYUMBANI MWAO KWA SABABU HAKUNA MTU ANAYETAKA KUWA NJE USIKU WA GIZA HATARI. KWA MIAKA MINGI, WANANCHI WA AMA WAMEKUWA NA WASIWASI NA HOFU.



AMA IMEKUWA KATIKA UGOMVI MKALI NA WA MUDA MREFU NA KIJIJI JIRANI CHA ZUTA. HAKUNA ANAYEJUA JINSI UGOMVI HUO ULIVYOANZA, INGAWA KILA KIJIJI KINAKILAUMU KINGINE. WATU WENGI WAMEKUFA NA MALI KUHARIBIWA KATIKA VIJIJI VYOTE VIWILI. VIJIJI VYA AMA NA ZUTA VILIVYOKUWA MAJIRANI WALIOISHI KWA AMANI, VIMEKUWA MAADUI WAKUBWA WASIOTAKA KUSULUHISHA MGOGORO WAO KWA NJIA YA AMANI.



FAMILIA KUTOKA AMA, BWANA NA BIBI MUSA NA WATOTO WAO WAWILI, WANAJIANDAA KWA USIKU MREFU USIO WA UHAKIKA UNAOKARIBIA.



Harakisha Yohana na uwafungie ng'ombe. Inatubidi kuingia nyumbani haraka; huenda maharamia wa Zuta watatokea leo usiku.

Hanna, nisaidie kuingiza ndani kuni na maji. Inatubidi kutayarisha chakula mapema na kujiandaa kulala.



BAADAYE, FAMILIA HIYO ILIPOKUA INAKULA, WANAJADILIANA KUHUSU MATATIZO YAO KUHUSU USALAMA.

Baba, kwa nini watu wa Zuta ni maadui zetu?



Shida ilingia walipoanza kuwa na choyo na kuamua kukiteka kisima cha pekee katika eneo hili.



Baba, lakini pia nimesikia kuwa wapiganaji wetu waliteka maeneo ya kuwindia.



Ni kweli Hanna, lakini hatukuanzisha mgogoro. Walianza wao, ikabidi tulipishe kisasi.



Lakini haya yataisha lini? Nimechoshwa na kutishwa au kuogopeshwa wakati wote.



Sielewi maana yake ni nini. Juzijuzi, nilikutana na mtoto kutoka Zuta nilipokuwa nikichunga ng'ombe wetu. Alionekana hana ubaya na sikuona shida ya kuwa marafiki naye.



La, huwezi kufanya hivyo! Hatuwezi kuchanganyika na wezi wale mpaka wakiachilie kisima.



Na sisi tutaachia maeneo ya kuwindia?



Sikiliza Yohana! Usijaribu kunizidi maarifa. Maliza chakula ukalale.



Ndiyo, baba.



WAKATI HUOHUO, BAADHI YA WANAKIJJI WA ZUTA WANAJIANDAA KWA USIKU, LAKINI KWA NJIA TOFAUTI. WAMESHIKA SILAHA ILI KUPAMBANA NA MAJIRANI ZAO WA AMA.



KIKUNDI HICHO KILIELEKEA KWA ARI KWA MAADUI ZAO WA MUDA MREFU, TAYARI KUSHAMBULIA.


Wakati umefika wa kuwafunza wale wezi wa Ama adabu tena.

Nahitaji mtoto mtumwa wa kunichungia mbuzi wa baba yangu na pengine wa kucheza naye.

Nitankamata mke mwingine leo usiku. Mke wangu ameanza kuzeeka.




BILA YA KUELEWA HATARI INAYOWAKABILI, WANANCHI WA AMA WANAPIKA VYAKULA VYAO NA KUJIANDAA KULALA.



WAKATI HUOHUO, BILA KUJULIKANA NA WAZUTA, MVULANA WA AMA ANAFUATILIA KILA HATUA YAO KUTOKA MAHALI ANAPOJIFICHA PORINI.

LAKINI KWA BAHATI MBAYA, ANAKANYAGA JIWE AMBALO NI LEGEVU NA KWA HIVYO KUGUNDULIWA.



ANAPOONA HATARI INAYOMKABILI, MVULANA HUYO ANAKIMBIA KUELEKEA AMA HUKU AKIFUKUZWA NA WAZUTA.



KWA BAHATI NZURI, MVULANA HUYO ANAELEWA VIZURI ENEO HILO.

PUNDE ANAFANIKIWA KUWAKWEPA WAZUTA.



NISAIDIENI! NISAIDIENI! WAZUTA WANAKUJA!



KELELE ZA MVULANA HUYO ZA KUOMBA MSAADA ZINAWAZINDUA WAPIGANAJI WA AMA KUJA KUMWOKOA.



GHAFLA, KIJIKI CHA AMA KINAKUWA UWANJA WA VITA. WAPIGANAJI WA AMA HAWAJAJIANDAA NA HAWANA SILAHA KAMA WAZUTA...



... MARA WANARUDISHWA NYUMA. BAADHI YAO WANAFULU KUJIFICHA PORINI HUKU WENGINE WANAKAMATWA.



BILA YA WAPIGANAJI WAO, WANANCHI WA AMA WANAKAMATWA NA WAZUTA. WAZUTA WANAWAPIGA BILA HURUMA NA KUWACHUKUA BAADHI KAMA MATEKA. KELELE ZA MAUMIVU NA UCHUNGU MKALI ZINATAWALA USIKU.



SIKU INAYOFUATA.....

WANANCHI WA ZUTA WANASHEREHEKEA USHINDI WAO. MATEKA WOTE WANATOLEWA HADHARANI ILI WATU WAWAONE. MIONGONI MWAO NI HANNA, BINTIYE MUSA. CHIFU ANAWAHUTUBIA WATU WAKE.

Habari za asubuhi wanakijiji wenzangu? Kama mnavyoona, leo ni siku maalumu kwetu sote. Mbali na kuwa mvua imetoshwa, tumeshinda vita vya kishujaa na kukamata mateka.



Zuta oyeee!!!



Adui daima ziii!!!




Nataka huyu awe mke wangu wa pili. Nilimkamata mimi mwenyewe.



WAKATI HUOHUO, WANANCHI WA AMA WANAOMBOLEZA. CHIFU WAO ANAWALIWAZA NA MGENI AMEKUJA KUWATIBU WALIOJERUHIWA.

Wanakijiji wenzangu, tumepata pigo jingine kubwa kutoka kwa maadui zetu wauaji. Sasa lazima tuchukue hatua. Wakati umefika wa kuwafyeka maharamia wa Zuta na kuwatokomeza wote. Kuna mwenye maoni?



Ili kuwaadhibu vilivyo, lazima tulenge wanawake na watoto. Ni rahisi kuwapata.




Nadhani tutie sumu kisima walichotupokonya. Hilo litawafunza adabu.



Pia ni lazima tuwauwe wanyama wao na kuchoma mimea yao.



Bila shaka, hayo yatawaathiri sana Wazuta. Lakini jiulizeni, je, ni haki kuwatendea hayo binadamu wenzako?



Bila shaka ni haki. Walitufanyia vivyo hivyo. Lazima tuwashambulie. Tusipofanya hivyo watahiani sisi ni waoga na watatushambulia tena.



Vizuri, ni sawa kujihami, lakini kuna haja gani ya kuwashambulia wale wasiopigana, kama vile wanawake na watoto?

Hiyo sio hoja! Hawakuhurumia yeyote miongoni mwetu.



Inabidi tujali. Kwa nini watoto, wanawake na wazee waathirike na vita visivyowahusu? Utamaduni na mila zetu haziruhusu hayo!



Nakubali! Pia sidhani ni lazima tufanye mambo kama vile kutia sumu katika kisima. Hicho kitakuwa kitendo kibaya na cha ukatili. Watu wote, wakiwemo wale wasiopigana, watataabika.



Aidha, tutaishia kuwauwa watu wetu wenyewe kama dada yangu HANNA, aliyetekwa nyara na Wazuta.

Ni kweli Yohana. Hatuna budi kufikiria jambo hili kwa makini kabla ya kuchukua hatua yoyote.



Kuna haja gani ya kufikiria? Tukusanye silaha, twende Zuta na kulipisha kisasi sasa hivi!



Lakini hayo ndiyo wanayoyatarajia; kwa hiyo watakuwa wamejiandaa. Napendekeza, chifu wetu ateue kikundi cha watu ili kupanga hatua yetu itakayofuata.



WANAKIJIJI WENGI WANAKUBALIANA NA PENDEKEZO LA MZEE, NA MKUTANO UNAFUNGWA.



WAKATI HUOHUO KATIKA KIJIKI CHA ZUTA

SHEREHE ZIMEKWISHA NA WANAKIJIJI WANAJIANDAA KULALA. HANNA AMECHUKULIWA HADI NYUMBANI MWA ALIYEMTEKA NYARA.

Hii inahuzunisha. Yeye bado ni mtoto kama kaka yangu na mimi.


Anaonekana hana raha hata kidogo.

Masikini mtoto huyu. Anapaswa kuwa na familia yake.

Atakuwa mke wangu mzuri hivi karibuni.



Haya watoto, wakati wa kulala umewadia. Maria, mpeleke mtumwa wangu mdogo chumbani mwenu. Kwa sasa atalala sakafuni.



Haya wasichana, usiku mwema. Tutaonana asubuhi.



MARA TU BAADA YA MLANGO KUFUNGWA, MARIA ANAMKARIBISHA HANNA WALALE KITANDANI. HANNA ANASITA, LAKINI MWISHOWE ANAKUBALI.



Nasikitika sana. Lazima unaogopa sana.

Najisikia ovyo. Sijui kama nitaonana na familia yangu na marafiki zangu tena.



Usikate tamaa. Pengine watu wazima wataona haja ya kukuruhusu kwenda nyumbani hivi karibuni. Kwa sasa tujiandae kulala.



BAADAYE, USIKU HUO.....

Maria, u macho?

Ko! Ko!
Ko! Ko!



Ndiyo, ingia Juma, lakini taratibu.



Nyie wasichana, tunahitaji kuzungumza. Mnajua, nadhani wanayofanya watu wazima hapa na katika Ama si mambo mazuri.



Sawa Juma, tufanyeje? Unajua, hatutakiwi kuwa na sauti. Kama watu wazima wanavyosema, "Watoto wanapaswa kuonekana tu na wala sio kuongea".



Hawataki tuongee, ingawa wanafurahia sisi kupigana vita vya watu wazima. Haya yote ni makosa. Maria, wewe na mimi hatungetaka kuwa katika hali kama ya Hanna; kwa hiyo, kwa nini tusimsaidie kutoroka?

Lakini atatorokaje? Kuna kiza na baridi, na walinzi wengi.



Tunaweza kusubiri mpaka mapambazuko wakati ambapo kuna mwangaza zaidi na walinzi wanasinzia.

Hilo ni wazo zuri. Tunaweza kumtorosha kupitia dirishani na kumwonyesha njia ya kurudi kijijini mwao.



Wazo zuri. Tufanye hivyo mapema na turudi kabla mtu yeyote kugundua kwamba Hanna hayupo.

Nyie wawili ni watu mahiri. Sijui niwashukuru vipi.




Kwa sasa, usijali kuhusu shukurani. Omba Mungu mradi wetu ufanikiwe. Sasa laleni. Lazima tuamke mapema. Usiku mwema.




BAADAYE KUNAPOPAMBAZUKA...

WALE WATOTO WATATU WANATOROKA KIMYA KIMYA KUTOKA NYUMBANI. KILA JAMBO LINAKWENDA KAMA ILIVYOPANGWA. MLINZI ANASINZIA SANA NA KWA HIVYO WANAFANIKIWA KUMPITA.



HATIMAYE WANAKIONA KIJIKI CHA AMA KWA MBALI. NI WAKATI WA KUAGANA.

Kijiki chenu kile pale Hanna.



Sijui niwashukuru vipi. Wazazi wangu na kaka yangu Yohana hawataamini!



Je, Yohana ni kaka yako? Nilikutana naye majuzi na ni mtu mzuri kweli. Nafurahi kuwa utafika nyumbani hivi karibuni. Lakini inakubidi ukimbie sasa kabla ya kukutwa!

JUMA NA MARIA WANAMPUNGIA HANNA MIKONO YA KWAHERINA KUHARAKISHA KURUDI NYUMBANI



KATIKA KIJJI CHA AMA...

MAMA YAKE HANNA AMEAMKA MAPEMA LEO ILI KUPIKA CHAI. WAKATI AKIENDELEA NA KAZI YAKE ANAFIKIRI KWA MAJONZI KUHUDU BINTI YAKE ALIYETEKWA NYARA.



Masikini mwanangu! Sijui kama nitamwona tena. Lazima ajione mpweke sana.

ANAPOWAZA HAYO HANNA ANAWASILILI NYUMBANI.



Mama! Mama! Nafurahi sana kukuona!


Hanna! Umerudi Asante Mungu!



BAADA YA KUKUTANA, FAMILIA INAINGIA NYUMBANI AMBAMO HANNA ANAELEZA KISA CHA KUTOROKA KWAKE.



HABARI ZA KUTOROKA KIAJABU KWA HANNA ZINAENEA HARAKA KATIKA AMA. WATU WOTE WAMEFURAHI NA KUSHANGAA KUWA YEYOTE KATIKA ZUTA ANGEWEZA KUFANYA MAMBO MAZURI.



LAKINI MTU MMOJA HAFURAHI



Majambazi hawa wanajaribu kutudanganya tu. Wakati umefika wa mimi kuwafunza Wazuta hawa wauaji funzo kamili.

Nilijua kuwa lazima kuwe na Wazuta wazuri.

Mzuta mzuri ni yule aliyekufa!








SIKU IFUATAYO KATIKA ZUTA....

MARIA NA JUMA WAMETUMWA KISIMANI KUTEKA MAJI NA KUWANYWESHA NG'OMBE WAO



BAADA YA KUTEKA MAJI NA KUHAKIKISHA KUWA NG'OMBE WAMEKUNYWA VYA KUTOSHA, WATOTO WANARUDI NYUMBANI

Natumai Hanna alifika nyumbani salama.

Hata mimi natumai hivyo. Lakini hakuna haja ya kumfikiria. Pengine hatutaonana naye tena.



Inasikitisha sana. Nilimpenda sana.

Hatujui mambo yakavyokuwa. Labda kuna siku vita vitakwisha na tutaweza kuwa marafiki.



LAKINI MARIA NA JUMA WANASHANGAA. HANNA NA YOHANA WANAOTOKA MADUKANI WANAONEKANA MBELE YAO.

Hanna! Ni vizuri mno kukuona.

Hujambo Yohana? Ni vizuri kukuona tena.



Alah! Mambo ni mazuri.
Ni vizuri kurudi nyumbani.
Yohana nami tulitaka kuonana
na nyinyi ili kuwashukuru.



Nyie ni watu wa ajabu
sana. Bado siamini
mliyomfanyia dadangu.

Ah! Usijali. Nina
hakika hata nyinyi
mnetufanyia vivyo
hivyo.



Laiti wazee
wangeacha vita hivi
visivyo na maana.



Sawa, tukiwa watu
wazima, tutawaonyesha
namna ya kufanya
mambo vizuri zaidi.



Ndio, lakini kwa sasa
tuondoke kabla mtu
mzima yeyote hajatuona.
Kuweni na tahadhari.
Tutaonana.



Kabla hamjaondoka, mnaweza
tupatia maji?



Bila shaka! kuna maji
ya kumtoshia kila
mtu.



BAADAYE...

YAELEKEA KUNA JAMBO LILILOHARIBIKA HUKO ZUTA. WANAKIJIJI WENGI NI WAGONJWA NA WOTE WANALALAMIKA KUUMWA NA TUMBO. HAKUNA ANAYEJUA KUNA NINI WALA LA KUFANYA.



Pengine ni kitu fulani tulichokula.
Labda bucha alimchinja ng'ombe mgonjwa.



Lazima tuchukuwe hatua!



Familia yangu yote inaugua
na zahanati yetu haiwezi
kutusaidia.

Baba, nilisikia kwamba
kuna mtu fulani huko Ama
ambaye anawasaidia
kupata nafuu wagonjwa na
watu walioumia. Tunaweza
kumwagiza.



Usiwe mpumbavu, wewe. Iwapo mtu huyo yuko
Ama, yuko upande wao na kwa hiyo, hawezi
kutusaidia.



Nimesikia kwamba anafanya kazi na shirika linalojulikana kama Msalaba Mwekundu. Wanamsaidia mtu yeyote mwenye shida bila ya kupendelea.

Unajuaaje yote haya Juma? Nafikiri unajua pia namna msichana wetu mtumwa alivyotoroka.



Nyote angalieni! Nimeipata chupa hii kisimani. Inaelekea kuna mtu aliyetia maji yetu sumu.



Lazima ni wale wahuni wa Ama. Twendeni tukawaagamize.

Subiri! Tufikirie kupona kwanza na wala sio kwenda vitani. Labda tumwagize yule mfanyakazi wa Msalaba Mwekundu.



Kama mtemi wa kijiji hiki, nitakwenda. Nitatuma ujumbe kwa Mtemi wa Ama ili tukutane karibu na Kisima.

Lakini tutamtuma nani ambaye hatashambuliwa?



Hilo ni wazo zuri. Sidhani watahambulia mtemi, lakini inabidi kutahadhari



MIPANGO INAFANYWA NA WATEMI WAWILI HATIMAYE WANAKUTANA.

Sijui ni nani aliyefanya jambo hilo, lakini kwa vyovyote vile, ni vibaya sana. Nitazungumza na watu wangu. Haya yamepita mipaka. Inabidi vijiji vyetu vikutane haraka ili kujadili matatizo yetu. Kwa sasa, lazima uende kuwasiliana na Msalaba Mwekundu ili watembelee kijiji chako na kuwasaidia wagonjwa.



MARA BAADA YA MKUTANO WA WATEMI, MFANYIKAZI WA MSALABA MWEKUNDU ANAWASILIZUTA ILI KUWASAIDIA WAGONJWA.



BAADA YA SIKU CHACHE, MKUTANO KATI YA AMA NA ZUTA UNAFANYIKA KISIMANI.



Tumekusanyika hivi leo ili kujadili namna tunavyoweza kutanzua matatizo yetu. Matukio ya hivi majuzi katika vijiji vyetu viwili yamesababisha madhara yasiyo na maana kwetu.



Nakubaliana nawe. Tunaweza kuwa maadui, lakini sote ni binadamu na inabidi tuheshimu utu wetu, hata tunapopigana.



Sawa. Sote tumekosea. Wakati wa ujana wangu, tulishambulia wapiganaji na wala si mtu yeyote.



Sote tumefanya mambo ambayo ni kinyume na mila na desturi zetu. Kwa mfano, zamani hatukutumia watoto kupigana vita vyetu. Watoto wanapaswa kuwa shuleni.




Sijui ni nani aliyefanya hayo, lakini ni wazi kwamba mtu fulani kutoka Ama alitia kisima chetu sumu.



Na kwa kufanya hivyo ameishia pia kuwanywesha sumu watoto wetu wawili, Hanna na Yohana.



Pengine kutia sumu kisimani halikuwa jambo la maana. Nafurahi kwamba hakuna mtu hata mmoja aliyefariki.



Tunashukuru Mungu kuwa Msalaba Mwekundu walikuwa karibu kusaidia vijiji vyetu vyote viwili.



Labda tutafute njia za kukomesha uhasama baina yetu. Kwa mfano, tungekuwa tunatumia kisima pamoja hakuna ambaye angekitia sumu. Kuna maji ya kumtoshia kila mtu.



Ni kweli. Tunaweza kuzungumza kuhusu jambo hilo. Kwa sasa, wale wanaonelea kwamba tuchukue hatua zaidi ili kuwalinda wale wasiopigana, wanyooshe mikono.



Nadhani mkutano huu ni mwanzo mzuri.
Tuzungumze kuhusu namna tunavyoweza
kukabili tofauti zetu. Labda kuna siku ambapo
hatutaweza kushirikiana kuhusu kisima tu bali
pia kuhusu maeneo ya kuwindia.



Labda kuna siku vijana kutoka vijiji vyetu viwili wataweza kuoana.



UKURASA WA WALIMU

Walimu Wapendwa,

Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (ICRC) nchini Kenya, ikisaidiana na wanafunzi na Walimu, imetayarisha kitabu hiki cha hadithi kwa picha ili kitumiwe katika shule za msingi. Lengo ni kuwaarifu, kuwaelimisha na kuwaburudisha wanafunzi wa madarasa ya juu ya shule za msingi, huku wakifahamishwa Sheria ya Kibinadamu ya Kimataifa (IHL), yaani sheria za kimataifa zenye lengo la kupunguza mateso miongoni mwa watu wakati wa vita.

Wajibu wa ICRC ni kusaidia na kulinda wanaokumbwa na migogoro ya kivita. Kupitia shughuli zake, inafanya kazi ili kuhakikisha kuwa utu wa wanaokumbwa na vita unaheshimiwa na kwamba mahitaji yao ya kimsingi yanatimizwa. Aidha, ICRC inaeneza maarifa ya IHL miongoni mwa wapiganaji, wanasiasa na sekta nyingine za jamii ili kuleta ufahamu wa haki za kimsingi za wanaokumbwa na vita. Mwisho, ICRC inafanya kampeni ili kupunguza matumizi ya zana na mbinu za vita zinazosababisha mateso yanayokithiri kwa binadamu.

Tumejaribu kukifanya kitabu cha "Vita vya Vijiji" kiwe rahisi kueleweka na cha kuvutia. Hata hivyo, mchango wa walimu ni muhimu sana ili kuhakikisha kuwa masuala yaliyogusiwa yanaeleweka vizuri kwa wanafunzi. Kutokana na sababu hiyo, tunawaomba mtusaidie kueleza na kuisitiza ujumbe wa kibinadamu wa kitabu hiki cha hadithi kwa picha kwa kutayarisha shughuli za ziada. Mnaweza kufanya hivyo kwa kutumia ipasavyo mila, desturi na utamaduni wenu au mnaweza kutumia shughuli zilizopendekezwa kwenye ukurasa huu.

Chama cha Msalaba Mwekundu kinashughulika sana nchini mwenu. Wasiliana nacho ili uone namna unavyoweza kusaidia katika shughuli zake za kibinadamu.

ICRC inawatakiwa nyinyi na watoto wenu wakati mzuri na wa furaha mnaposoma kitabu hiki cha hadithi kwa picha. Iwapo mna maoni au mapendekezo yoyote wasiliana nasi kwa anwani iliyotolewa katika ukurasa wa nyuma wa kitabu hiki.

SHUGHULI YA 1: UFAHAMU

Yafuatayo ni maswali machache unayoweza kutumia ili kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu hadithi:

1. Je, vijiji viwili katika hadithi vinaitwaje?
2. Kwa nini vijiji viwili hivyo viliingia vitani?
3. Hanna alipatwa na nini wakati wa vita?
4. Hanna alisaidiwa na nani na kwa njia gani?
5. Ni nani aliwasaidia wagonjwa katika vijiji vyote viwili?
6. Kisima kilifanyiwa nini? Matokeo yake yalikuwa nini?
7. Kwa nini vijiji vyote viwili viliamua kufanya mkutano?
8. Mkutano huo ulifanyika wapi?
9. Ni nani waliosababisha matatizo kati ya vijiji viwili (Jadili).
10. Ni nini ujumbe wa hadithi? (Jadili)

SHUGHULI YA 3: IGIZO:

Wanafunzi wanaweza kutayarisha igizo kuhusu hadithi; au, unaweza kuwasaidia kutumia hadithi katika utamaduni, mila na desturi zao. Kwa mfano, iwapo hakuna visima katika eneo lenu, mtu kutoka Ama angetia sumu mimea ya chakula mashambani mwenu.

SHUGHULI YA 3: SAFARI YA UTAFITI CHINI YA USIMAMIZI WA MWALIMU

Iwapo mna muda wa kutosha, nyinyi walimu na wanafunzi wenu mnaweza kutayarisha safari ya kiutafiti ya eneo lenu. Lengo ni kuchunguza namna zamani wakazi wa eneo hilo walivyoshughulikia migogoro kati yao na maadui zao. Kwa mfano wanafunzi wanaweza kuwahoji wazee wa jumuiya au viongozi wa kiasili ili kupata taarifa zaidi.

SHUGHULI YA 4: INSHA:

Wanafunzi wanaweza kutumia mawazo waliyopata katika shughuli ya 3 katika kuandika insha kuhusu mada ya migogoro ya kivita na matokeo yake. Kwa mfano, wanaweza kuandika kuhusu swali: "Je, vita viwe na mipaka?"

MAJIBU YA FUMBO LA PICHA KWENYE UKURASA WA WANAFUNZI

1. Rangi nyeusi kwenye kofia ya askari wa Ama (Picha B).
2. Mtu kutoka Zuta hana bendeji (Picha A).
3. Mmea karibu na kisima hauna jani (Picha A).
4. Mtu anayecheka hana jino (Picha B).
5. Ndege walioko mbali (Picha B)
6. Hanna hana kidole (Picha B).
7. Mtoto wa kiume hana Sikio (Picha A).
8. Mtemi hana mkongojo (Picha A).
9. Mwanaume hana mguu (Picha A).
10. Maneno, "Mwisho" hayana herufi H

UKURASA WA WANAFUNZI

Shughuli zifuatazo zinahusu hadithi uliyoisoma na zimekusudiwa kukuelimisha na kukuburudisha. Unaweza kuzifanya peke yako au kwa kushirikiana na rafiki yako au marafiki zako:

FUMBO LA MANENO:

Katika fumbo la maneno lifuatalo jaribu kutafuta maneno kumi na moja yaliyoorodheshwa. Maneno yote yametoka katika hadithi ya "Vita vya Vijiji" uliyoisoma. Yameandikwa yakielekea nyuma, mbele, mlalo mshazari, chini na juu. Mfano wa neno linaloelekea juu, "Mapambano" limetolewa kukusaidia.

Maneno

1. Mapambano
2. Vita
3. Kijiji
4. Uchungu
5. Sumu
6. Kisima
7. Katuni
8. Hanna
9. Yohana
10. Msalaba
11. Mwekundu

M	J	I	J	I	J	I	K	O	M
W	O	T	A	T	I	V	Y	N	S
E	I	H	T	I	D	A	O	A	A
K	A	T	U	N	I	A	H	B	L
U	G	N	U	H	C	U	A	M	A
N	H	O	J	H	A	N	N	A	B
D	A	K	I	S	I	M	A	P	A
U	I	C	R	C	Z	U	T	A	O
Z	A	M	U	U	M	U	S	M	M

GUNDUA TOFAUTI!

Huenda picha zilizoonyeshwa hapa (A na B) zikaonekana kama zimefanana kabisa. Hata hivyo, kuna tofauti kumi kati ya picha hizo. Unaweza kuzitambua tofauti hizo zote?





ULINZI:

ICRC inasikiliza waliokumbwa na vita ambao haki zao zimekiukwa wakati wa vita.



HATUA ZA KUZUIA:

ICRC inajitahidi kueneza ufahamu wa Sheria ya Kibinadamu ya Kimataifa miongoni mwa Wapiganaji na jamii kwa ujumla.



KIZUIZINI:

ICRC hutembelea watu waliotiwa kizuizini wakati wa migogoro ya kivita ili kuhakikisha kwamba wanatendewa mambo kwa namna isiyokiuka heshima ya binadamu.



MATIBABU:

ICRC huwatibu wale waliojeruhiwa vitani na hujaribu kuhakikisha kuwa kila mmoja wao anapata matibabu hata wakati wa vita.



UTAFUTAJI:

ICRC hutumia huduma zake za utafutaji na kuwasaidia maelfu ya watu kukutana tena hao wakiwa ni pamonja na watoto, wanaojikuta pweke na ambao wametengwa na familia zao kutokana na migogoro.

ICRC INASTAWISHA HESHIMA YA WATU WALIO KATIKA SHIDA KUTOKANA NA MIGOGORO YA KIVITA




USAIDIZI:

ICRC husaidia mamilioni ya wanaokumbwa na vita kote duniani waliohamishwa au ambao hawawezi tena kujikimu kwa kuwapatia chakula, malazi, mavazi na vifaa vingine muhimu kwa maisha.



MAJI NA MAKAZI:

ICRC husaidia wanaokumbwa na vita kupata maji ya kutosha ya kunywa vilevile kuwa na usafi unaostahili.



USHIRIKIANO:

ICRC inafanya shughuli zake nyingi kwa kushirikiana karibu sana na vyama vya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu vya Kitaifa vya nchi inakofanya kazi. ICRC pia inatoa msaada wa kiufundi na kifedha ili kusaidia kustawisha vyama vya Msalaba Mwekundu au Hilali.

ANWANI:

ICRC Nairobi Regional Delegation, Denis Pritt Rd., P.O. Box 73226, Nairobi, Kenya; Tel.: (254) 020 2723963, 2713367, 351374; Fax: (254) 020 2715598; E-mail: nairobi.nai@icrc.org; ICRC Dar Es Salaam, Ali Hassan Mwinyi & Ruhinde Rd., Plot No. 87, P.O. Box 23431, Dar Es Salaam, Tanzania; Tel.: (255) 222667/ 668552; Fax: (255) 222 667 797, E-mail: dar_es_salaam.dar@icrc.org



ICRC